**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**

**OFISI YA RAIS**

TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA

**HALMASHAURI YA WILAYA BUKOBA**

SIMU... +255 (028) 2220 287,
Nukushi: 0282221836
Barua pepe: ded@bukobadc.go.tz

S.L.P. 491,
**BUKOBA.**

## TARATIBU ZA KUFUATA ILI KUPATA KIBALI CHA UJENZI

Kulingana na sheria ya ujenzi wa majengo kwenye Mamlaka za Upangaji ambazo ni Mamlaka za Miji Midogo, Halmashauri za Miji, Manispa na Ma-jiji si ruhusa kwa mtu yeyote kujenga au kuanza jengo jipya bila ya:

(i) Kutuma maombi kwa mamlaka ya mji
(ii) Kuwasilisha michoro ya jengo na kumbu kumbu husika.
(iii) Kupata kibali kwa maandishi 'kinachoitwa “kibali cha ujenzi.”

Kibali cha Ujenzi *(Building Permit)* ni nyaraka ya ki-Sheria inayotolewa na Mamlaka za Upangaji *(Planning Authorities)* ambazo ni Mamlaka za Serikali za Mitaa *(The Local Government Authorities)* ili kuruhusu Ujenzi mpya, kubomoa, kuondosha, kuongeza, au kufanya marekebisho makubwa. Kufanya hivyo kutasaidia kurekebisha kasoro zinazoweza kuathiri uimara wa jengo na mifumo mingine ya maji safi na taka, tahadhari za moto, umeme, usalama wa jamii na uharibifu au uchafuzi wa mazingira.

Sanduku la Posta 491 Bukoba, Kagera
**Simu:** 028 2220287, **Nukushi:** 028 2221839 **Barua pepe:**ded@bukobadc.go.tz, **Tovuti:** bukobadc

Kwa mujibu wa Vifungu 124 na 125 vya Kanuni za Sheria ya Serikali za Mitaa (Mamlaka za Miji) (Udhibiti Uendelezaji), Sura 288 (GN 242 ya mwaka 2008), Ujenzi wowote ndani ya Mamlaka za Upangaji ambazo ni Mamlaka za Miji Midogo, Halmashauri za Miji, Manispa na Ma-jiji ni lazima upate kibali cha Ujenzi kutoka kwenye Mamlaka husika.

## JINSI YA KUWASILISHA MAOMBI YA KIBALI CHA UJENZI

Baada ya michoro kukamilika iwasilishwe ikiwa kwenye majalada kwa namna ambayo inawezekana kufunguliwa na kusomeka. Michoro hiyo iwasilishwe kwa utaratibu ufuatao

i. Nakala tatu (3) za michoro ya majenzi (Architectural Drawings) na kugongwa muhuri wa msanifu majengo (Architects).

ii. Nakala mbili (2) za michoro ya majenzi (Structural Drawings) na kugongwa muhuri wa mhandisi wa ujenzi (kwa majengo ya ghorofa).

## MICHORO ILIYOANDALIWA IONYESHE NINI ?

Michoro iliyoandaliwa inatakiwa ionyeshe mambo yafuatayo:

i. Namna jengo litakavyokuwa (plans sections, elevation, foundation and roof plan).
ii. Namba na eneo la kiwanja kilipo.
iii. Jina la mmiliki ardhi inayohusika.
iv. Jina la mchoraji ujenzi na anwani.
v. Ukubwa wa jengo kwa mita za mraba.
vi. Ujazo wa kiwanja (Plot coverage).
vii. Uwezo (Plot ratio)
viii. Matumizi yanayo kusudiwa.
ix. Idadi ya maegesho yatakayo kuwepo.
x. Umbali wa jengo kutoka kwenye mipaka ya kiwanja (atbacks)
xi. Mfumo wa kutoa maji taka hadi kwenye mashimo

**VIAMBATANISHO**

Muombaji wa kibali cha ujenzi anatakiwa  kuambatanisha nyaraka zifuatazo.

i. Fomu za maombi zilizo jazwa kwa usahihi
ii. Hati ya mmiliki wa kiwanja au barua ya toleo
iii. Picha nne (3) za passport size zinazofanana
iv. Kumbu kumbu zingine zinazohusu kiwanja hicho kama hati ya mauzo, makabidhiano n.k
v. Nakala za risiti ya kodi ya kiwanja ya sasa (Kwa kiwanja kilichopimwa).
vi. Mabadiliko ya matumizi ya ardhi kama muombaji amebadilisha matumizi ya awali
vii. Hati ya kiwanja (Certificate of occupancy) au Mkataba wa Mauziano uliopitishwa katika serikali ya Kijiji na Muhtasari wa Kijiji/Mtaa uliopitisha mauziano hayo.
viii. Uthibitisho wa Uraia (Kitambulisho cha Uraia/Cheti cha kuzaliwa/Passport ya kusafiria) ziwe nakala halisi (Certified copy of the Original)
ix. Ramani ya kiwanja iliyosajiliwa (Kwa maeneo yaliyopimwa).

**FAIDA ZA KUWA NA KIBALI CHA UJENZI**

i. Kujenga nyumba ambayo imethibitishwa kitaalamu kuwa ni salama.
ii. Kuwa na mazingira bora kwa kuwa na mji uliopangwa.
iii. Kuepuka hasara na usumbufu unaoweza kutokea iwapo ujenzi umefanyika bila kibali ikiwa ni pamoja na kushtakiwa mahakamani kuvunjiwa na kulipa gharama za uvunjaji.
iv. Kulipwa fidia iwapo jengo litabomolewa kwa sababu maalum.
v. Kuweza kupata mkopo kutoka Taasisi za fedha.

**MUDA**

Michoro itaidhinishwa ndani ya siku saba (7) toka mwombaji awasilishe maombi ya jengo la chini (mfuto). Na siku kumi nne (14) jengo la ghorofa. Aidha ndani ya muda huo mwombaji ataarifiwa sababu za michoro kutoidhinishwa kupata kibali cha ujenzi.

**Maombi na viambatanisho vyote viwasilishwe katika Ofisi ya Mkurugenzi Mtendaji Halmashauri ya Wilaya ya Bukoba**

Sanduku la Posta 491 Bukoba, Kagera
**Simu:** 028 2220287, **Nukushi:** 028 2221839 **Barua pepe:**ded@bukobadc.go.tz, **Tovuti:** bukobadc